

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



TAARIFA KWA UMMA

**UTEUZI WA WAJUMBE WA KAMATI YA USHAURI KATIKA
MASUALA YA ELIMU KATIKA MUUNGANO**

1. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Selemani Saidi Jafo (Mb.) ameteua Wajumbe saba (7) kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la kuteua wajumbe hao ni kupata ushauri wa kitaalamu kuhusu uboreshaji wa elimu katika Muungano ili sekta zinazohusika na masuala ya elimu za Tanzania Bara na Zanzibar ziweze kushauriwa ipasavyo.
2. Uteuzi huo umefanyika ikiwa ni hatua ya kushughulikia maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbali kuhusu tofauti ya ufaulu wa wanafunzi wa Shule za Sekondari za Tanzania Bara na Zanzibar kwa matokeo mbalimbali ya Kidato cha Nne na Sita. Aidha, Wabunge mbalimbali wamekua wakiwasilisha hoja hiyo wakati wa mjadala wa bajeti ya mwaka 2021/22 wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).
3. Kamati iliyoteuliwa itafanya kazi kwa siku thelathini na tano (35) na kuwasilisha taarifa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ili kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi waweze kukaa na Mawaziri wanaohusika na masuala ya elimu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwashauri namna bora ya kuboresha elimu pande zote mbili za Muungano.
4. Wajumbe walioteuliwa ni:-

- i. **Prof. Alexander Boniface Makulilo**, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Taaluma, Utafiti na Huduma kwa Umma) - **Mwenyekiti**
- ii. **Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.)**, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – **Makamu Mwenyekiti**
- iii. **Bw. Abdulmarik Mollel**, Mkurugenzi Mtendaji wa *Global Education Link* – **Katibu**
- iv. **Bw. Khalid Bakari Hamrani**, Mkurugenzi wa Uratibu wa Shughuli za Serikali, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi – **Mjumbe**
- v. **Dkt. Charles Msonde**, Katibu Mtendaji wa NECTA – **Mjumbe**
- vi. **Bw. Jaled Mveli**, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI – **Mjumbe**
- vii. **Bw. Said Hamad Shehe**, Mkufunzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Zanzibar (IPA) - **Mjumbe**

Imetolewa na



Lulu Mussa
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Zanzibar
17 Mei, 2021